



JARIDA MAAALUM

Toleo la 22 | Mei, 2021

OFISI YA WAZIRI MKUU

NDANI...

MAJALIWA AAGIZA UCHUNGUZI WATENDAJI WIZARA YA FEDHA

Waziri Mkuu, Mheshimwa Kassim Majaliwa amewasimamisha kazi Mkaguzi Mkuu, Mkaguzi Msaidizi pamoja na baadhi ya watendaji wa Wizara ya Fedha na Mipango ili kupisha uchunguzi wa tuhuma za matumizi mabaya ya fedha za umma zinazowakabili.

MAJALIWA: TUTAENDELEA KUSIMAMIA BEI NZURI YA MAZAO

Waziri Mkuu Kassim Majaliwa amesema kuwa Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Mhe. Samia Suluhu Hassan itaendelea kusimamia bei nzuri ya mazao kwa wakulima nchini.



Ofisi ya Waziri Mkuu



owm_tz



www.pmo.go.tz

JARIDA LA MTANDAONI



MAJALIWA: TUTAENDELEA KUSIMAMIA BEI NZURI YA MAZAO

Waziri Mkuu Kassim Majaliwa amesema kuwa Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Mhe. Samia Suluhu Hassan itaendelea kusimamia bei nzuri ya mazao kwa wakulima nchini.

Ametoa kauli hiyo (Alhamisi, Mei 27, 2021) wakati akijibu swali la Mbunge wa Kyerwa Innocent Bilakwate katika kipindi cha Maswali ya Papi kwa Papo kwa Waziri Mkuu Bungeni jijini Dodoma.

Mbunge huyo alitaka kufahamu mpango wa Serikali wa kuhakikisha zao la Kahawa linakuwa na soko la uhakika.

"Kahawa ni miongoni mwa mazao ya kimkakati ambayo yanalimwa na jamii pana hivyo Serikali itaendelea kusimamia ushirika, masoko ili wakulima waweze kulipwa kwa wakati".

Aidha, Waziri Mkuu amesema kuwa pamoja na kutafuta changamoto ya masoko, pia Serikali

imeendelea kutekeleza mkakati wa uanzishwaji wa viwanda ndani ya nchi ili zao la kahawa liweze kuongezewa thamani na kuwa na masoko ya uhakika.

Wakati huo huo, Waziri Mkuu amesema kuwa Serikali itaendelea kuweka mikakati ya kuhakikisha inawalinda raia na mali zake ili wanaendesha kazi zao kwa amani na utulivu.

"Hata Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kupitia hotuba yake moja ya kitaifa, amewaonya wote wanaofikiria huu ni wakati wa kufanya maovu nchini na amewataka wote wanaofikiria kufanya hivyo waache mara moja, haya pia ni maagizo kwa vyombo vya ulinzi na usalama kuwachukulia hatua wanaosababisha madhara ya usalama kwa watanania"

Pia, Waziri Mkuu ametoa wito kwa watanania kushiriki katika suala la ulinzi na usalama kwa kutoa taarifa kila wanapoona kuna dalili za uvunji-fu wa amani.

MAJALIWA: WATAFITI, WABUNIFU ONGEZENI KASI YA TAFITI



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa amewataka watafiti na wabunifu nchini kuongeza kasi ya kufanya tafiti ili nchi iende sambamba na mabadiliko yanayotokea ulimwenguni kote.

Ametoa wito huo Mei 24, 2021 wakati wa ufunguzi wa maadhimisho ya sita ya wiki ya utafiti na ubunifu yakiyofanyika katika viwanja vya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Jijini Dodoma.

“Mabadiliko haya ya teknolojia yanatokea kwa kasi kubwa ulimwenguni yanachochewa na mwenendo wa maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Hivyo basi, nasi hatunabudi kujipanga vyema ili kuedana na kasi hiyo”.

Amesema kuwa ni lazima watafiti na wabunifu katika sekta zote wachukue hatua za makusudi katika kubuni na kutumia teknolojia zinazoibuka kwa ajili ya kuleta maendeleo endelevu ya viwanda na jamii yetu.

“Wakati tukifanya hayo yote, ni muhimu pia kujitarisha kutumia kikamilifu matokeo ya tafiti zetu kama fursa au bidhaa adimu ya biashara”

Aliongeza kuwa baada ya tafiti hizo wahakikishe matokeo ya tafiti yanapelekwa kwa umma ili uweze kufaidika na matokeo hayo kwa kupata suluhisho za changamoto mbalimbali zinazoikabili Jamii badala ya kuyafungia makabati.

Aidha, Waziri Mkuu amevitaka vyuo vikuu vyote nchini kuweka utaratibu wa kufanya utafiti na kisha kuonesha matokeo ya tafiti ili kusaidia kuimarisha uhusiano wa karibu baina ya vyuo na soko la ajira.

Kadhalika Waziri Mkuu ametoa wito kwa wenye viwanda kutoa ufadhili wa tafiti na bunifu zinazohusiana na bidhaa zinazozalishwa katika viwanda vyao

“Tumieni vizuri wataalamu wa vyuo vyetu kwani wanaweza kuleta majibu ya changamoto mbalimbali katika uzalishaji bidhaa, masoko ya bidhaa, mahitaji ya wateja na mambo mengine mengi”

Pia, Waziri Mkuu amekitaka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kutekeleza mpango wa vitengo vya

utafiti kwenye mikoa ikiwemo cha mkoa wa Lindi ambako tayari walikwisha pewa eneo.

Naye Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Joyce Ndalichako amesema kuwa Serikali itaendelea kuimarisha tafiti ili taifa liweze kunufaika na teknolojia ya kisasa na kutoa huduma kwa jamii.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa na Waziri wa Elimu, Sayansi na Tekinolojia, Profesa Joyce Ndalichako (wa pili kushoto) wakipata maelezo kutoka Mhadhiri Mwandamizi katika Chuo Kikuu cha Dar es salaam, Paul Onyango (kushoto) kuhusu uzalishaji wa vifaranga vya kambale katika Maadhimisho ya Sita ya wiki ya Utafiti na Ubunifu ya Chuo Kikuu cha Dar es salaam, kwenye viwanja vya Maktaba Mpya ya Chuo Kikuu hicho jijini Dar es salaam.



MAJALIWA: NACTE VISAIDIENI VYUO KUTOA ELIMU YENYE KUKIDHI MAHITAJI

Waziri Mkuu Kassim Majaliwa ameliagiza Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) liimarisha usimamizi na kuvisaidia vyuo kutoa elimu inayozingatia viwango vya ubora na vyenye kukidhi mahitaji ya soko ya ajira la sasa na lijalo.

Amesema kuwa ni wajibu wa vyuo hivyo kuhakikisha vinatoa elimu bora ili kuwafanya wahitimu wake wawe mahiri na kukidhi mahitaji ya nchi na pia kuwawezesha kujajiri wao wenyewe.

Ametoa agizo hilo (Ijumaa, Mei 28, 2021) wakati akifungua Maonesho ya Pili ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi katika uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma.

Amesema kuwa vyuo vya elimu na mafunzo ya ufundi vinapaswa kutumia fursa ya maonesho hayo kujitathmini na kujipima ili kuona ni kwa

namna gani vinaweza kutoa Elimu na Mafunzo ya Ufundi bora yanayokidhi mahitaji ya sasa ya soko la ajira na kutoa fursa kwa vijana kujajiri.

“Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025 imeweka wazi kuwa elimu ni kipaumbele cha juu kwani ndiyo kitovu cha kuleta mabadiliko ya kiuchumi kwenye jamii”.

Aidha, Waziri Mkuu amesema kuwa ulimwenguni kote elimu na mafunzo ya ufundi na ufundi stadi hujulikana kwa mchango wake mkubwa katika ukuaji wa maendeleo ya viwanda, uchumi na ustawi wa jamii. “Vyuo na taasisi zinazotoa elimu hii ni lazima vihakikishe vinatoa elimu bora inayokidhi viwango na mahitaji ya soko la sasa la ajira”



MAJALIWA: MARA WEKENI MKAKATI WA KUITANGAZA MBUGA YA SERENGETI

WAZIRI MKUU Kassim Majaliwa amewataka viongozi wa Mkoa wa Mara na Watendaji katika Sekta ya Utalii wabadilike na waweke mkakati wa kuitangaza mbuga ya Serengeti ili kuweza kuvutia zaidi watalii na kuitambulisha mbuga hiyo kuwa iko mkoa humo.

Amesema Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Mhe. Samia Suluhu Hassan inaboresha mazingira ya uwekezaji na biashara ili kuvutia uwekezaji utakaoinua uchumi wa nchi na watu na mwongozo huo ni sehemu ya utekelezaji wa azma ya Serikali ya kuvutia uwekezaji na kuimarisha biashara.

Waziri Mkuu ametoa agizo hilo (Ijumaa, Mei 28, 2021) wakati akizindua Mwongozo wa Uwekezaji wa Mkoa wa Mara katika Ukumbi wa Bishop Rudin

uliopo katika viwanja vya Mwembeni mjini Musoma. Waziri Mkuu ametumia fursa hiyo kuwaagiza viongozi wa mkoa huo wahakikishe watendaji, wataalamu na wananchi wanakuwa nyenzo ya kurahisisha kazi ya kuvutia uwekezaji.

“Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa hakikisha watendaji wote wa mkoa wanausoma na kuuelewa ipasavyo mwongozo huu. Hakikisha watendaji wako wanatekeleza majukumu yao kwa weledi, uadilifu na uaminifu ili kufikia malengo yaliyokusudiwa”.

Waziri Mkuu amesema mkoa huo una fursa nyingi za uwekezaji ambazo endapo zitatumika vema, zinaweza kuipaisha nchi kimaendeleo. “...Nitoe wito kwa uongozi mzima wa mkoa uhakikishe unaratibu vilivyo shughuli za uzalishaji hasa wa malighafi, bidhaa na huduma mbalimbali kwa ajili ya wananchi na mahitaji ya viwanda vya ndani.



MAJALIWA AAGIZA UCHUNGUZI WATENDAJI WIZARA YA FEDHA

Waziri Mkuu, Mheshimwa Kassim Majaliwa amewasimamisha kazi Mkaguzi Mkuu, Mkaguzi Msaidizi pamoja na baadhi ya watendaji wa Wizara ya Fedha na Mipango ili kupisha uchunguzi wa tuhuma za matumizi mabaya ya fedha za umma zinazowakabili.

Akizungumza katika Kikao Kazi na Waziri wa Fedha na Mipango, Kaibu Mkuu, Manaibu Katibu Wakuu na Watendaji Waandamizi wa Wizara hiyo kwenye ukumbi wa Hazina jijini Dodoma Mei 27, 2021, Mheshimiwa Majaliwa amemuagiza Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Kamishna wa Polisi CP Salum Rashid Hamdun kufanya uchunguzi kuhusu tuhuma hizo na ikithibitika kwamba tuhuma si za kweli wahusika watarejeshwa kazini.

Mheshimiwa Majaliwa alizitaja baadhi ya tuhuma hizo kuwa ni malipo yaliyofanyika Machi 31,

Mwaka huu kupitia vocha 30 ya sh.milioni 251 yakielezwa kuwa ni malipo maalum bila kutaja kazi hiyo maalum ni kazi gani na nani aliifanya hiyo kazi.

Amesema siku hiyo hiyo ya Machi 31 pia zililipwa sh. milioni 198.8 kwa madai kuwa ni posho ya honoraria.

Mheshimiwa Majaliwa amesema Aprili 8 mwaka huu watumushi 27 wa Wizara hiyo walilipwa sh. milioni 44.5 zikiwa ni posh ya kazi maakum ya wiki nne. Pia Aprili 13 mwaka huu zililipwa sh. Milioni 155.2 kwa watumishi 68 ikiwa ni posho ya ya kazi maalum ya wiki tatu.

Aidha, Aprili 30 mwaka huu zililipwa sh. milioni 43.9 kwa ajili ya kuandaa mpango wa kuhifadhi mazingira na siku hiyo hiyo zililipwa sh miloni 14.4 kwa ajili ya siku ya wanawake. Fedha nyingine sh.

Milioni 43 zililipwa siku hiyo na kufanya jumla ya malipo yaliyolipwa siku hiyo kuwa shilingi mikio-ni101.8.

Amesema kuwa, mei 1 asubuhi mwaka huuzililipwa sh. milioni 184.1 na mchana zililipwa sh. milioni 264 zikiwa ni malipo ya kazi maalum. "Sisi tulikuwa Mwanza tunasherehekea siku ya wafanyakazi duniani nyinyi hapa ndani mnalipana posho" Aliongeza kuwa Mei 3 mwaka huu zililipwa sh. milioni146.5 kwa watumishi 125 zikiwa ni malipo ya kuandaa Mpango Kazi wa Manunuzi kazi ambayo ni sehemu ya majukumu yao ya jila siku. Tarehe hiyohiyo zililipwa sh. milioni 171.2 kwa ajili ya kuandaa nyaraka za Bunge.

Mheshiniwa Majaliwa amesema sh. milioni 155 zililipwa kwa baadhi ya watumishi zikiwa ni posho

yakuandaa miongozo wakazi. " Yaani hii kazi ya ukaguzi ineliowa kwenye maeneo manne, huu ni utaratibu wa wa wapi? Mnazidi kutupunguzia imani, na sijaongeeke eneo la kuhamisha mafungu na utaratibu kuhamisha fedha kisha mnakwenda kuzichukuwa huko mlikozihamishia."

Mheshimiwa Majaliwa amewataka watendaji wa Wizara hiyo kujenga uaminifu kwa wanaokusanya mapato kwa kufanya kazi kwa uaminifu na alitahadharisha kuwa watakaondekea kuchen na pesa za umma hatua kali zitachukuliwa dhidi yao.

Aidha, Waziri Mkuu aliwapongeza watendaji wengine wa wizara hiyo ambao wameendelea kufanya kazi kwa weledi "na nimesema hapa si wote wenzenu wachache wanatumia vibaya nafasi zao kutuchafua wizara ya fedha"



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akizungumza na Waziri wa Fedha na Mipango, Katibu Mkuu na Naibu Makatibu Wakuu pamoja na Watendaji Waandamizi wa Wizara hiyo katika kikao cha kazi kilichofanyika kwenye ukumbi wa Hazina Jijini Dodoma, Mei 27, 2021.



KATIBU MKUU
Ofisi ya Waziri Mkuu
2 Mtaa wa Relini, S.L.P 980
40480 Dodoma,
Baruapepe: ps@pmo.go.tz, Simu:+255262322480
Fax:+255262324534, Tovuti: www.pmo.go.tz